# BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU ZANZIBAR

**MWONGOZO WA UTOAJI MIKOPO KWA WAOMBAJI WAPYA KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024**

## 1.0 UTANGULIZI

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ) ni Taasisi ya Serikali inayojitegemea ikiwa chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) na imeanzishwa chini ya Sheria Namba 3 ya mwaka 2011. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar inajukumu la kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo kwa lengo la kuufanya utaratibu wa utoaji mikopo kuwa endelevu.

***Waombaji mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2023/2024 wanatakiwa kusoma na kufuata taratibu za maombi katika Mwongozo huu wa mwaka wa masomo 2023/2024.***

## 2.0 MAELEKEZO MUHIMU KWA WAOMBAJI WAPYA

Waombaji wote wa Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2023/24 maombi yao yanapaswa kuyawasilisha kupitia mfumo maalum wa maombi ya mtandaoni unaojulikana ***ZHELB Online Loans Application System (ZOLAS)***.

Mfumo wa **ZOLAS** umeunganishwa na mifumo ya Tasisisi nyengine za Elimu ya Juu, zikiwemo Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu (TCU), Baraza la Mafunzo ya Ufundi (NACTVET), Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA).

Aidha, ZOLAS imeunganishwa na mfumo wa Mamlaka ya Usajli wa Matukio Maalum ya Kijamii ya Zanzibar (ZCSRA) inayotoa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, na mfumo wa malipo wa Serikali (ZANMALIPO).

Ili kuweza kutuma maombi kwenye mfumo wa ZOLAS, waombaji wote wanatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i. Kuwa na Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

ii. Kuhakikisha kuwa nambari ya mtihani wa kidato cha nne iwe sawa na nambari aliyoituma kuwasilisha maombi ya kujiunga na chuo.

iii. Kuhakikisha kuwa majina yake matatu yanayotumika kwenye Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi na kidato cha nne yanalingana.

iv. Wahitimu wa nje ya Tanzania wawe na ithibati ya ulinganisho (Equivalence) kutoka NECTA kwa kidato cha nne na sita, NACTVET kwa Stashahada na TCU kwa Shahada.

v. Wahitimu wa Stashahada wawe na *Award Verification Number* (AVN) kutoka NACTVET).

vi. Kuwa na baruapepe (*email*) binafsi na ambayo haitobadilika kwa wakati

wote.Waombaji wanasisitizwa kuhifadhi vizuri neno siri (*password*) zao

vii. Kuwa na nambari ya simu ya mkononi iliyosajiliwa na kutumika wakati wote. Mwombaji atatakiwa kuweka nambari yake ya simu kwa kutumia "*country code*" (**255XXXXXXXXX**).

viii. Kuhakikisha kufanya malipo stahiki ya maombi kwenye akaunti ya BMEJZ baada ya kufungua akaunti (profile) kwenye mfumo wa maombi wa ***ZOLAS*** na kupatiwa nambari ya kumbukumbu (control number) ya kufanyia malipo hayo.

ix. Kurudufu (*scanning*) nyaraka zote muhimu zinazohitajika wakati wa maombi zikiwemo barua za kukubaliwa kujiunga na masomo, matokeo (*transcript*) na vyeti vya kumalizia masomo kwa waombaji shahada ya pili/uzamili nashahada ya tatu/uzamivu.

x. Waombaji wote wa vyuo vya nje ya nchi wanatakiwa kuambatisha barua za udahili (*Admission letter*) pamoja na barua kutoka Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu (TCU) zinazoridhia kujiunga na Chuo na kusoma fani husika ***(No Objection Certificate)***.

xi. Maombi ya mikopo yanapaswa kukamilika, taarifa sahihi na kuwasilishwa ndani ya wakati.

## 3.0 JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Maombi ya mikopo yatumwe kupitia tovuti ya BMEJZ ***(https://zhelb.go.tz)*** na kubonyeza kitufe cha ***Online Loan Application System***.

Aidha, waombaji wanaweza kutuma maombi yao kupitia kiunganishi (*link*).***zolas.zhelb.go.tz/zolas***.

Ili kuweza kuwasilisha maombi hayo, kila mwombaji anatakiwa kukamilisha hatua zifuatazo:

### 3.1 Kujisajili

Baada ya kubofya kiunganishi ***zolas.zhelb.go.tz/zolas*** utafunguka ukarasa ambao mwombaji atapaswa kujaza nambari ya Kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi na nambari ya mtihani wa kidato cha nne.

***Angalizo:***

- Majina matatu ya muombaji yanayotumika kwenye kitambulisho cha Mzanzibari na kidato cha nne yawe yanalingana. Vyenginevyo utashindwa kusajiliwa na kuendelea na hatua nyengine zinazofuata.
- Nambari ya mtihani wa kidato cha nne iwe sawa na nambari iliyotumika kuwasilisha maombi ya kujiunga na chuo.

Baada ya kukamilika kwa hatua hii, mwombaji ataingiza nambari yake ya simu ya mkononi, anuani ya baruapepe na nambari ya mtihani wa kidato cha sita akiwa ni mhitimu wa kidato cha sita au nambari maalum ya utambulisho (***Award Verfication Number – AVN***) kwa mhitimu wa Stashahada/Diploma.

## 3.2 Kufungua Akaunti (ZHELB Online Student Account)

Wakati wakujisajili katika Mfumo wa ZOLAS, Mwombaji atatumiwa nambari maalum ***(Verification Code)*** kwenye baruapepe aliyowasilisha. Mwombaji atapaswa kuitumia nambari maalum ***(Verification Code)*** kwa kuweka neno siri (create password) ambayo ataitumia kwa kuingia kwenye Mfumo wa ZOLAS. Katika Mfumo wa ZOLAS, Mwombaji atapaswa kutumia jina la utambulisho (username) ambayo ni nambari yake ya Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi

## 3.3 Kutuma maombi

Ufunguzi wa akaunti unamwezesha mwombaji kutuma maombi kwa kufuata maelekezo yaliyopo na kujaza kikamilifu kila kipengele husika ikiwa ni pamoja na waombaji wa mikopo kulipa **TZS 30,000/-** ambazo ni gharama za maombi zinazolipwa kupitia mitandao ya simu ya mkononi. Malipo yatafanyika baada ya mwombaji kupatiwa nambari maalum (***control number)***. Malipo yatakayofanyika bila ya kutumia nambari maalum (***control number***) hayatozingatiwa.

Kwa maelezo zaidi tembelea ***https://zhelb.go.tz*** au piga simu namba *+255777607509/ +255777348967*

**SIFA ZA KUPATA MIKOPO**

Sifa za waombaji wa mikopo ambao maombi yao yanaweza kuzingatiwa wakati wa uteuzi zimetajwa kwenye kifungu cha 20 cha Sheria Na. 3/2011 ya BMEJZ.

Sifa hizo ni zifuatazo:

a) Awe Mzanzibari mwenye kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.
b) Awe amewasilisha maombi yake kupitia mfumo wa mtandao wa maombi wa BMEJZ ndani ya muda maalum uliowekwa.
c) Awe amepata alama nzuri za ufaulu zinazomruhusu kupata udahili kwenye chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa na mamlaka husika nchini.
d) Awe ameomba fani za vipaumbele vya Taifa (**Angalia Kiambatisho Na. 1**).
e) Asiwe na mkopo au udhamini wa masomo kutoka taasisi nyengine.
f) Ukomo wa umri wakati wa kutuma maombi usiozidi miaka 35 kwa Mwombaji wa shahada ya kwanza, miaka 45 kwa mwombaji wa shahada ya uzamili na miaka 47 kwa mwombaji wa shahada ya uzamivu.
g) Mwombaji anayedaiwa na BMEJZ awe ameshaanza kulipa deni lake kwa angalau asilimia 25 ya deni lote bila ya kusita kwa malipo ya deni ya kila mwezi. Ikumbukwe kuwa malipo ya asilimia 25 ya mkopo wa awali siyo dhamana ya kupangiwa mkopo.
h) Waombaji wa vyuo vya nje wapate ithibati ya kukubaliwa kujiunga na chuo ***(No Objection Certificate)*** kutoka Tume ya Vyuo Vikuu ya Tanzania (TCU).

Wanafunzi wanaoendelea na masomo ambao ni wanufaika wa mikopo hawahitajiki kuwasilisha maombi mapya ya mikopo. Wanafunzi hao wanapaswa kujaza mikataba kwa kila mwaka mpya wa masomo unapoanza pamoja na kuwasilisha matokeo ya mitihani.

## 4.0 KUTANGAZWA MAJINA YA WAOMBAJI WALIOTEULIWA

Orodha za majina ya waombaji walioteuliwa kwa kila chuo na fani yatatangazwa kupitia tovuti za BMEJZ na WEMA katika mwezi wa **Oktoba 2023**. Aidha, kila mwombaji atakayeteuliwa atatumiwa taarifa ya uteuzi kupitia baruapepe au ujumbe mfupi wa simu na kupitia akaunti yake aliyoombea mkopo.

## 5.0 KUJAZA MIKATABA

Mkataba ni hati ya makubaliano kati ya BMEJZ na mwanafunzi ambapo BMEJZ itampatia muombaji mafao stahiki baada ya muombaji huyo kutimiza masharti yote yaliyoainishwa kwenye Mkataba.

### 5.1 Mikataba ya Waombaji Wapya

Waombaji wapya walioteuliwa wa mikopo na ufadhili wa masomo wa SMZ watapaswa kujaza mikataba na kulipia ada ya Mkataba ya **TZS 35,000** ili kuweza kunufaika na mafao yanayotolewa na BMEJZ. Mwombaji aliyeteuliwa atapaswa kuingia kwenye akaunti yake aliyoitumia wakati wa kuwasilisha maombi ya mikopo au ufadhili wa masomo wa SMZ.

Kupitia akaunti hiyo, mwombaji atapatiwa nambari maalum ya kumbukumbu ya kufanya malipo ***(Control Number)*** kabla ya kuendelea na hatua nyengine za kujaza mikataba.

### 5.2 Mikataba ya Wanufaika Wanaoendela na Masomo

Wanufaika wa mikopo na ufadhili wa masomo wa SMZ wanaoendelea na masomo mwaka 2023/24 katika Taasisi mbalimbali za Elimu ya Juu za ndani na nje ya nchi ambao hawakutuma maombi yao kwa njia ya mtandao, wataendelea kujaza mikataba inayopatikana katika ofisi za BMEJZ za Unguja na Pemba.

Wanafunzi waliojaza mikataba yao ya awali kwa njia ya mtandao, watapaswa kujaza mikataba mipya kwa kuhuisha taarifa zao kulingana na mwaka wa masomo uliopo.

## 6.0 MAFAO KWA WAOMBAJI WA MIKOPO

### 6.1 Utaratibu wa malipo ya ziada ya ada (topup)

Katika mwaka wa masomo 2022/23 BMEJZ imeanzisha utaratibu mpya wa kufidia kwa wanafunzi waliopata mkopo ya HESLB na ZHELB kwa pamoja. Kutokana na mkataba wa makubaliano kati ya ZHELB na HESLB wanafunzi hao wanatakiwa kubakia katika mkopo wa HESLB.

Ila kutokana na changamoto ya kupata asilimia ndogo ya ada imepelekea wanafunzi hao kuchagua mkopo wa ZHELB na sio HESLB.

Utaratibu huu wa topup utawasaidia wanafunzi wote wenye changamoto ya ada. BMEJZ haitakuwa na jukumu lolote jengine isipokuaka ada tu.

Sifa za malipo ya ziada kwa ada (topup)

a. Awe amepata mikopo yote miwili ZHELB na HESLB
b. Awe katika fani za uhandisi wa ndege, afya au ualimu sayansi.
c. Awe amejaza fomu Nam. 5 inayopatikana kwa afisa mikopo wake (loan officer) ndani ya muda uliowekwa. Fomu hiyo itakua sehemu ya mkataba wake.
d. Ada yake iwe inaanzia milioni 4 kwa mwaka.

### 6.2 1.1 Vipengele vya Mafao

Kwa kuzingatia uhitaji wa waombaji wa mikopo na ufadhili wa masomo wa SMZ, BMEJZ inalipa gharama za masomo kwa baadhi ya mafao kama ifuatavyo:

| Na. | Mafao kwa waombaji wa mikopo vyuo vya ndani | Mafao kwa waombaji wa mikopo wa vyuo vya nje |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya masomo na mitihani | Ada ya masomo na mitihani |
| 2. | Posho la chakula na malazi | Posho la chakula na malazi |
| 3. | Malipo ya ziada ya ada kwa kozi maalum kwa wateuliwa wa HESLB (TOPUP) | Tiketi ya ndege |
| 4. | Bima ya afya | Bima ya afya |

### 6.3 Utaratibu wa Malipo

Posho la chakula na malazi zitalipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki ya mwanafunzi. Ada ya masomo na mitihani yatalipwa moja kwa moja kwenye Taasisi husika.

**Tanbihi:** inasisitizwa mwanafunzi kuwasilisha nambari sahihi za akaunti na iliyo hai itakayolipwa posho la chakula na malazi.

## 7.0 WAOMBAJI WA MIKOPO NJE YA NCHI

***Kwa mwaka 2023/24, waombaji wa masomo katika Taasisi za Elimu ya Juu za nje ya nchi watakaoteuliwa kupata mikopo ni wale amabao fani za masomo yao ni za Vipaumbele vya Taifa na hazifundishwi au zina ushindani mkubwa katika Taasisi za Elimu ya Juu za Tanzania hasa katika kada maalum za afya, uhandisi, mafuta na gesi, kilimo, uvuvi, tiba za mifugo na uchumi wa buluu.***

Waombaji wapya wa mikopo wanaotarajia kujiunga au wanaoendelea na masomo katika taasisi za elimu ya juu nje ya Tanzania, wanapaswa kuchagua ama kulipwa ada ya masomo

au posho la kujkimu pekee. Hakuna mwanafunzi atakayelipiwa ada ya masomo na posho la kujikimu kwa pamoja.

Aidha, malipo ya ada yamewekwa ukomo maalum unaolingana na **US$ 3,200** kwa mwaka na tofauti ya ada itakayojitokeza italipwa na mwafunzi husika. Utaratibu huu unatekelezwa ili kumjengea mnufaika wa mikopo ya BMEJZ mazingira wezeshi ya kurejesha deni lake bila ya usumbufu baada ya kuhitimu masomo yake.

## 8.0 UTARATIBU WA MKOPO KWA WANAOREJEA MWAKA

Wanafunzi watakaorejea mwaka husika wa masomo watalazimika kuwasilisha barua rasmi kutoka chuoni inayothibitisha uwepo wa taarifa hizo. Uongozi wa BMEJZ ukuridhia mwanafunzi husika atapatiwa nyongeza ya mwaka mmoja katika miaka yake ya masomo.

> **Tanbihi:** Fursa hiyo ya kupatiwa mkopo kwa mwanafunzi itakuwa ni kwa mara moja tu katika miaka yake ya masomo.

## 9.0 RUFAA KWA WAOMBAJI WALIOKOSA MIKOPO

Wanafunzi watakaokosa kuchaguliwa kupata Mikopo ya BMEJZ na hawakuridhika na matokeo wanapaswa kuwasilisha malalamiko yao kwa Mkurugenzi, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ndani ya mwezi mmoja baada ya kutoka matokeo ya uteuzi.

## 10.0 WADHAMINI WA WANUFAIKA WA MKOPO NA WAJIBU WAO

Kila muombaji wa mkopo atakayeteuliwa atalazimika kuwa na wadhamini wawili. Wadhamini wana wajibu wa kuthibitisha usahihi wa taarifa za waombaji na kutoa taarifa zao binafsi ambazo zitawasilishwa wakati wa kujaza mkataba wa mkopo kabla ya kusaini.

Aidha, Wadhamini wanatakiwa kuhakikisha mikopo inarejeshwa na wanapaswa kufahamu mahali wakopaji walipo na ikitokea mnufaika hajamaliza kulipa, mdhamini atalazimika kulipa mkopo huo.

## 11.0 UREJESHAJI MIKOPO

Baada ya kuhitimu au kusitisha masomo ya elimu ya juu, mnufaika wa mkopo atatakiwa kurejesha mkopo kwa kiwango maalum cha malipo kwa kila mwezi au kulipa deni lake kwa mkupuo akiwa na uwezo wa kufanya hivyo.

**ANGALIZO:** Mwombaji atakayetoa taarifa zisizo sahihi atakuwa amekwenda kinyume na taratibu za kanuni na anaweza kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na jina lake kufutwa katika waombaji walioteuliwa kupatiwa mikopo.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI,**

**BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU,**

**ZANZIBAR.**

**KWA MAWASILIANO**

*Email. info@zhelb.go.tz*
*Website: https://zhelb.go.tz*
*Mobile +255777607509/ +255777348967*

ANUWANI:

MKURUGENZI,
BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU,
P.O.BOX 3344,
ZANZIBAR.

**Kiambatisho Na. 1: FANI ZA KIPAUMBELE**

Uteuzi wa waombaji, mbali na kuangalia sifa za kitaaluma na vigezo vyengine, hufanywa kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa ambavyo hupitiwa upya kila baada ya muda. Fani za Vipaumbele vya Taifa kwa mwaka wa masomo 2023/24 vinajumuisha:

| SEKTA | FANI NA KIWANGO CHA KIPAUMBELE | | |
|---|---|---|---|
| | **DARAJA LA KWANZA** | **DARAJA LA PILI** | **DARAJA LA TATU** |
| **UALIMU** | Science and Mathematics | Curriculum Development | Learning Materials Development |
| | Early Childhood and Primary Education | School science Laboratory Management | |
| | Geography, English, Historyand Kiswahili | IT with Education in Science Subjects or Mathematics | |
| | Physical Education and Sport Professional | Education Administration, Management and Planning | |
| | Library and Information Studies | | |
| **AFYA** | Anaesthesiology | Cardiology | Biochemistry |
| | Dentistry | Dermatology | ENT |
| | Gastroenterology | Endocrinology | General Medicine |
| | Haematology | General Surgeon | Microbiology and virology |
| | Medical imaging and Radiology | Medical Emergency | Nephrology |
| | Neurology and Neurosurgery | Oncology | Pharmacy and Pharmacology |
| | Obstetrics and Gynaecology | Paediatric surgery | Plastic surgery |
| | Ophthalmology | Physiotherapy | Rheumatology, Allergy and Immunology |
| | Orthopaedic | Psychiatry | Nursing and Midwifery |
| | Urology | Pathology | Molecular Biology |
| | Health informatics | ICU podiatry | Biotechnology |
| | Diagnostic ultrasound | Biomedical engineering | |
| **ARDHI** | Cartography | Architecture | |
| | Geoinformatics | Quantity Surveying and Construction Economics | |
| | Land Management and valuation | Property and Facilities Management | |
| | Land Surveying | Interior design | |
| | Urban and Rural Planning | | |
| | Landscape architecture | | |
| | Sedimentology | | |
| | Housing and Infrastructure Planning | | |
| **NISHATI** | Petroleum Geology | Petroleum economics and finance | Petroleum Law |
| | Petroleum Chemistry | Radiation Protection | Accounting in Oil and Gas |
| | Petroleum Engineering | Renewable Energy and Atomic Energy | Operational and Supply Chain in Oil and Gas |

| SEKTA | FANI NA KIWANGO CHA KIPAUMBELE | | |
|---|---|---|---|
| | **DARAJA LA KWANZA** | **DARAJA LA PILI** | **DARAJA LA TATU** |
| | Geophysics/Geochemistry | Petroleum Data Management | Oil and gas management |
| | Petroleum Economics | | |
| | Environmental Engineering (Oil and Gas) | | |
| **BIASHARA** | Trade Economics | International Economy and Trade/Finance/Commerce | Trade Administration |
| | Metrology and Standardization | Entrepreneurship | |
| **VIWANDA** | Industrial Engineering (Production, Quality Assurance, Product Design) | Mining/Metallurgy Processing Engineering | |
| | Chemical Engineering | | |
| | Mechanical engineering | | |
| | Biological/Chemical Laboratories Technicians | | |
| **UTALII** | Tourism Marketing | Language Professions | Hotel Management |
| | Cultural heritage and Conservation | Tourism Management | House keeping |
| | Hospitality | Archaeology | |
| | Tourism Planning | | |
| **KILIMO, UFUGAJI, UVUVI NA FANI ZINAZOSHABIHIANA NA UCHUMI WA BULUU** | Aquaculture | Agro Forests | Agriculture Planning |
| | Irrigation Engineering | Animal breeding | Agronomy |
| | Plant Breeding | Animal Nutrition | Animal Husbandry |
| | Plant Pathology | Biotechnology | Fisheries Science |
| | Soil science Disciplines | Entomology | Marine Science |
| | Bio-processing and post-harvest | Food and nutrition | Seed Technology |
| | Veterinary | Horticulture | Microbiology |
| **FEDHA** | Financial Market and Investment | Insurance | Banking and Finance |
| | Financial Management | Procurement | Tax Management |
| | Programme Analysis | Risk and Damage Evaluation | |
| | Actuarial science | | |
| **USAFIRI NA MAWASILIANO** | Municipal and Industrial Services Engineering | Marine and Port Administration | Maritime law |
| | Civil engineering | Road Economists | Maritime Business and Management |
| | Electrical and Biomedical Engineering | Pilot and Aircraft Maintenance Engineering | |
| | Shipping and Port engineering/Nautical Architecture | Mechanical engineering | |
| | Marine engineering technology | Electrical engineering | |

| SEKTA | FANI NA KIWANGO CHA KIPAUMBELE | | |
|---|---|---|---|
| | **DARAJA LA KWANZA** | **DARAJA LA PILI** | **DARAJA LA TATU** |
| | Maritime Transport and Nautical Science | Organization and Management of International Traffic | |
| | Mechanical and Marine (Nautical) Engineering | Road Engineering and Construction | |
| **TEHAMA** | Computer and software Engineering | Computer Science | |
| | Information systems and networks | Information, Communication Technology (ICT) | |
| | Electronics and Telecommunication Engineering | | |
| **MAJI** | Water Resources and Irrigation Engineering | | |
| | Water management | | |
| **MAZINGIRA** | Natural Resources Management | Environment Impact Assessment | Environment Health Surveying |
| | Disaster and Risk Management | Environment Planning and Management | |
| | Aquatic environmental sciences and conservation | Waste Management | |
| | Environmental science and management | Water management | |
| **UCHUMI NA MIPANGO YA MAENDELEO** | Monitoring and Evaluation | Human Resource Management, | |
| | Specialized Economics (Educational health, development). | Planning and Project Management | |
| | Statistics | International Development Policy and Negotiation | |
| | Urban and Regional Planning | | |
| | Regional Development Planning | | |
| **NYENGINEZO** | Demography | Local Government | Mass Communication |
| | Law specialization (Maritime, Oil and Gas, Drafting, Contract) | | International Relations |

**TAREHE MUHIMU ZA MCHAKATO WA MAOMBI YA MIKOPO 2023/2024**

Julai 15 –Julai 19: Waombaji kusoma mwongozo kapitia *https://zhelb.go.tz*
Julai 19 - septemba 18: Maombi ya Mikopo kupokelewa kupitia Mfumo
Julai 31 – Agosti 05: Kutuma maombi kupitia maonesho (maisara)
*Link za kufanya maombi: https://zhelb.go.tz au*
*zolas.zhelb.go.tz/zolas*.
Vituo – Hub ya Skuli ya Jang'ombe Sekondari Unguja, skuli ya Regezamwendo Unguja
Chachani Maktaba kuu na Skuli ya Chasasa Wete Pemba
septemba 19: Mfumo kufungwa
Oktoba 2023: Matokeo ya uteuzi wa maombi ya Mikopo

**LIPA MKOPO NA WENGINE WASOME**